**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2026**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu: 0769209747**

**Mkuu wa Shule: 0769209747**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0765516413**

**Mwandamizi Taaluma: 0765419500/0682193951**
**Matron/Patron 0766249634/0759607388**

**Shule ya Sekondari JULIUS KAMBARAGE NYERERE,**

**S.L.P 435, TARIME.**

**Tarehe: .................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JULIUS KAMBARAGE NYERERE ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA MWAKA ...................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya HGL, HGK, HGFa na HGLi.

Shule ya Sekondari Julius Kambarage Nyerere ipo umbali wa Kilometa 25 Mashariki mwa Mji wa Tarime, Usafiri wa gari ndogo kutoka mjini TARIME unapatikana katika kituo cha mabasi TARIME mjini. Nauli ni Shilingi 6,000/- kwa magari ya abiria. Kwa wale wa kaskazini wakipitia Arusha na Moshi wakipitia Mbugani Serengeti yanapita Nyamongo, unashukia Nyamwaga, unaweza kumwambia dereva akushushe kwenye kibao cha shule Julius Kambage Nyerere (JK NYERERE) ipo mkabala na Ofisi za Halmashauri ya TARIME Vijijini.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............ Mwishoa kuripoti ni tarehe ……………….

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

i. Sare ya shule hii ni Sketi mbili kwa Wasichana moja ya rangi nyekundu na ya pili ya rangi ya Maruni, ndefu hadi chini ya kisigino mshono wa linda box kitambaa kizito. Kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni
ii. Mashati meupe aina halwa (*mawili yenye mikono mirefu*);
iii. Sare ya Michezo ni Sketi ya Blue na Tisheti ya Blue (**inapatikana shuleni kwa atakayehitaji**).
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; visiwe buti.
v. Soksi jozi nne (au zaidi) nyeupe ndefu ( Stocks) za shule;
vi. Kwa Waislamu shona kijuba cheupe kwa ajili ya kuvalia Sare ya shule, cheusi kwa ajili ya kuvalia Shamba dress.
vii. Masweta ya rangi ya bluu bahari na shingo ya V na nembo ya shule. **(yanapatikana shuleni).**
viii. Track suit ya blue yenye nembo ya shule kwa ajili ya usiku wakati wa baridi, iwe na upana wa kutosha na isiyoshika wala kubana mwili kwa atakayehitaji
ix. Tisheti (T-shirt) mbili zenye nembo ya shule moja Kijivu na rangi Nyeusi. (**zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji).**
x. Raba nyeupe za michezo pea mbili
xi. Kwa wale wenye matatizo ya kiafya **NI LAZIMA KUTHIBITISHWA NA DAKTARI KWA KUAINISHA CHANGAMOTO HIYO YA AFYA KWENYE FOMU AMBAYO IMEAMBATANISHWA)**
xii. Aje na masweta mazito meusi yasiyo na maandishi ya aina yoyote ile.
xiii. Aje na blanketi kwa ajili ya kujifunika wakati wa usiku na kujikinga na baridi.
xiv. Aje na dawa mbili ya Mbu(Hit/Rungu Spray ya mils 600 na kuendelea)
xv. Magauni/ Shamba Dress 2 (ndefu hadi miguuni kwenye kisigino) kitambaa Kizito **rangi ya blue Giza (Blue nyeusi)** kizito kisichopitisha Mwanga kwa ajili ya kuvaa wakati wa usafi na kazi za nje ya masomo.

**NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani shuleni isipokuwa nguo za shule tu. Kama rangi na mshono vitakuchanganya, unaweza kuvipata maeneo ya shuleni.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 (*Counter books quire four*);
ii. **Rimu/Ream ( Double A4)** tatu (3) kwa mwaka; Ream zingine tofauti na double A4 hazitapokelewa.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika, Vitabu vinavyopendekezwa ni kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania TIE.
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro liwe na vipimo vya futi 3 kwa 6 (**super banco**)
vi. Mashuka Jozi 3; jozi moja blue na mawili rangi ya pinki, blanket moja, mto na foronya ya rangi bluu na pinki, pia aje na chandarua kimoja chenye rangi nyeupe, Night dress nyeupe na Taulo za kike za kutosha.
vii. Nguo za ndani za kutosha kwani hali ya hewa ya huku ni ya mvua na baridi.;
viii. Ndala (kanda mbili) za kuogea rangi ya bluu.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 (moja lita 10 moja lita 20) zenye mifuniko pamoja na beseni la kufulia (karai);
xi. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake pamoja na kufuli za kufungia.
xii. Vifaa vya usafi;

| **HGK** | **HGL** |
|---|---|
| ➢ Skwiza 1 | Skwiza 1 |
| ➢ Jembe moja na mpini | Chelewa ya kusimama moja |
| ➢ Chelewa ya kusimama 1 | Jembe moja na mpini |
| ➢ Mifagio laini 1 | Mifagio mgumu 1 |

| **HGFA** | **HGLI** |
|---|---|
| ➢ Kwanja 1 | Reki 1 |
| ➢ Jembe moja na mpini | Chelewa ya kusimama. |
| ➢ Chelewa ya kusimama | Jembe moja na mpini |
| ➢ Dawa ya chooni lita 5 (nzito) | Dawa ya chooni lita 5 (nzito) |

**NB. Dawa za choo zinapatikana kwenye duka la shule ambazo ni nzito kwa atakayehitaji.**

XIV. Faili mbili (2) kwa kila mwanafunzi.

XV. Taa ndogo ya sola kwa ajili ya kujisomea wakati umeme ukikatika.

XVI. Tai yenye mistari ya rangi nyeupe na nyekundu au rangi ya maruni na nyeupe.

xvii. Kanga kwa aajili ya kuogea, **kumbuka vikoyi, masai shuka pamoja na mtandio haviruhusiwi.**

xviii. Fulana mbili nyeupe.

xix. Viatu vya kimasai kwa ajili ya kushindia vyenye mikanda miwili kwa aajiili ya kushindia na wakati wa chakula.

### 2.3 Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Mzazi unashauriwa kumkatia mtoto bima ya afya na aje nayo pindi anaporipoti shuleni.**
**Michango yote ilipiwe kwenye akaunti ya shule akaunti namba 30410008757 NMB jina la akaunti ni JK NYERERE SEC SCHOOL.**

### Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za shule na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

#### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Evening Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa katika mazingira ya shuleni na nje ya shule;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na Matroni.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).


- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**


**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule hairuhusiwi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali isainiwe na kugonga muhuri wa mganga Mkuu wa serikali.; NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI kuja na fomu hii ikiwa imejazwa na hautapokelewa usipokuja nayo.
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha ndogo nne (4) (passport size) za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
V. Kopi ya cheti cha kuzaliwa pamoja na results slip ya matokeo ya kidato cha nne.

**MIPAKA YA SHULE**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

i  i) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
ii  ii) Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu
iii  a) Ofisi ya walimu (staff room)
iv  b) Ofisi zingine za shule
v  c) Maabara
vi  d) Jikoni
vii  e) Nyumba za walimu / wafanyakazi wasio walimu

**NB Mwanafunzi hauruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wakimu na maeneo tajwa hapo juu isipokuwa kwa kibali maalumu. Mwanafunzi atakayekiuka utaratibu wa ruhusa uliowekwa adhabu yake ni pamoja na kurudishwa nyumbani au kufukuzwa shule.**

**UGONJWA**


i) Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika zahanati ya shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika hospitali ya serikali
ii) Mwanafunzi mwenye matatizo lazima amfahamishe matron/ uongozi wa shule, mara afikapo shuleni
iii) Wagonjwa wafike zahanati saa 1: 00 asubuhi kwa ajili ya matibabu kabla ya Kwenda darasani
iv) Mwanafunzi aje na bima ya afya (NHIF INAYOTUMIKA) au aje na fedha taslimu Tsh 50,400/= kwa ajili ya bima hiyo

**MUHIMU**

a. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi, mwanafunzi atavaa sare za shule muda wote awapo shuleni na asafiripo kuja shuleni au aendapo nyumbani.**
b. Kila mzazi /mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanae kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo na kumpa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi. Ruhusa ya kufuata fedha za matumizi haitolewi. Mzazi unakumbushwa kuwa kumpa mwanao fedha inayopita kiasi, kwaweza kuchangia kuporomoka kwa taaluma yake.
c. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Kila mara ahakikishe ni nadhifu kwa nywele fupi zisizozidi urefu wa sentimeta moja na nusu(1.5cm)
d. **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu akiwa shuleni. (HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU SHULENI)**

***TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU*.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**MELESIAN JULIUS GERALD**

**Mkuu wa Shule**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**
**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule:  0769209747**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0765516413**
- **Mwandamizi Taaluma: 0765419500/0682193951**
- **Mwandamizi Malezi: 076624963**

Mkuu wa Shule,

Shule ya Sekondari JULIUS KAMBARAGE NYERERE,

S.L.P. 435,

**TARIME**

**YAH: <u>BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII</u>**

Asante kwa barua yako Kumb.Na…………………ya tarehe ……………………………..

(a) Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha tano kwa mwaka……………
(b) Niko tayari/siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya JULIUS KAMBARAGE NYERERE Sekondari
(c) Nitahudhuria/Sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni
(d) Nikishindwa kuhudhuria bila sababu ya msingi nifukuzwe shule.
(e) Nitaleta/Sitaleta

    (i) Vitu vinavyohitajika kwa matumizi yangu
    (ii) Cheti cha Afya
    (iii) Fomu ya kuandikishwa na habari zangu za mzazi/mlezi wangu.

Asante.

…………………………….. ……………………….

**JINA LA MWANAFUNZI** **SAINI YA MWANAFUNZI**

**NB: Kama unakubali basi kata kwa kalamu sehemu ya kutokukubali.**

*Kiambatanisho i*

## FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM).

**JULIUS KAMBARAGE NYERERE SECONDARY SCHOOL**

**P.O. BOX 435,**

**TARIME**

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

The Medical Officer ……………………………….. From Headmistress,

(GOVERNMENT M.O) JULIUS KAMBARAGE NYERERE Secondary School,

Date: ………………………

Name of Student ……………………………………………………………............ Date ………………… Term ……… Year …………….. I shall be very grateful if you will kindly examine the above named student and give us a report regarding her fitness to undertake studies well in our school.

**A: PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL HISTORY**

| NO | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Tuberculosis | | | 7 | Kidney/ trouble | | | 13 | Operation | | |
| 2. | Asthma | | | 8 | Diabetes | | | 14 | Eye disorder | | |
| 3 | Pneumonia | | | 9 | Neverous breakdown | | | 15 | V.D | | |
| 4 | Heart trouble | | | 10 | Ear/Noise/Throat trouble | | | 16 | Disabled | | |
| 5 | Recurrent indigestion | | | 11 | Skin disorder/ disease | | | 17 | | | |
| 6 | Jaundice | | | 12 | Anaemia | | | 18 | | | |

**B: VITAL STATISTICS**

Age ……………….. Height ………………Weight …………….. Blood group …………………

Blood pressure ……………………….. Pulse rate …………………………..

Systolic …………………………………..Diastolic …………………………..

**C: MEDICAL EXAMINATION:**

| | REMARKS/TREATMENT |
|---|---|
| EAR | RT. LT………………… |
| VISION | RT. EYE LT. EYE |
| THROAT | |
| CHEST EXAMINATION | |
| ABDOMINAL EXAM. | LIVER SPLEEN |
| | OTHER COMMENTS |
| M.S. SYSTEM | UPPER LIMBS |
| | LOWER LIMBS |
| | SKIN |
| ANY OTHER FINDING | |

**D: LABORATORY EXAMINATIONS/INVESTIGATION:**

(1) STOOL: - Ova ………………………Leucocytes ……………………………………………

(2) URINALYSIS: PROTEIN ………………………………………………………………………

GLUCOSE ………………………………………………………………………

SEDMENT: - OVA ……………………Leucocytes ……………………

(3) Hb ………………………………………………………………………………………………………

(4) B/S ………………………………………………………………………………………………………

(5) VDRL ……………………………………………………………………………………………………

(6) WBC Total ………………………………………………………………………………………
Differential: N ……….. L …… M ……… E ……… B ……………

(7) X-ray Chest
(If necessary) ……………………………………………………………………………………

(8) ANY OTHER INVESTIGATION THAT SHOULD BE TAKEN INTO CARE
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………


**E. MEDICAL CERTIFICATE:**

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above named student and considered that he is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date: ……………………………….Station …….............................................................….

Dr’s Name: …….......................................................……………….Signature ……………………….…Stamp..............................




MELESIAN JULIUS GERALD,

Headmistress,

**JULIUS KAMBARAGE NYERERE SECONDARY SCHOOL.**

**0769209747**

***Kiambatanisho ii***

**a) HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI.**

1. Jina la kwanza ………………………………… Jina la kati ……………………..……..…
   Jina la mwisho ………………………………………………
2. Jina la Mzazi/Mlezi ………………………………………………………
3. Kama ni Mlezi: uhusiano ……………………………………………………………
4. Namba za simu za Mzazi/ Mlezi …………………………………………….
5. Anwani ya kudumu ya Mzazi/Mlezi ………………………………………..
6. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Kijiji cha ………………………………………………… Kata ya ………………………. Wilaya …………………….. Mkoa …………….
7. Dini ……………………………………… Dhehebu ……………………………..
8. Unaingia kidato cha ………………….. Tarehe/Mwaka ……………………
9. Shule ya sekondari uliyomalizia kidato cha nne ………………………………………….. Wilaya ……………………………………… Mkoa …………………………………
10. Kazi anayofanya Mzazi/Mlezi wako ni……………………………….…………… Mahali ……………………………
11. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa maelezo)
    - ❖ ………………………………………………………………………………………
    - ❖ ………………………………………………………………………………………
12. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari muhimu juu yako au masuala ya shuleni ni:-

| Jina la ndugu | Uhusiano | Namba za simu |
|---|---|---|
| i) | | |
| ii) | | |
| iii) | | |
| iv) | | |

13. Unalipiwa/utalipiwa michango na: Taja jina na anwani yake, au namba za simu ……………………………………………………………………….……………………………..
14. Taarifa za wazazi: A. Wapo ( ) B. Wamefariki ( ) (weka vema ( √ ) panapohusika)

15. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? ………………(ndiyo/hapana).

    ni ugonjwa upi ni wakudumu kwako? (unaohitaji uangalizi wa karibu/maalumu)

    ……………………………………….

16. Sifa maalumu kama unazo (kama vile uoni hafifu n.k)
    ……………………………………………………...

17. Nakiri kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni sahihi na Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kweli. Naahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe:…………………………………..Saini ya Mwanafunzi ……… ………………………

**b) MKATABA WA MWANAFUNZI WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

**Mimi (jina la mwanafunzi) ………………………………………………………………… nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Pia naahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya yoyote ya jinai niwapo shuleni hapo.**

**Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………**

**Saini ………………………………………. Tarehe ………………………………**

***Kiambatanisho iii***

**FOMU YA MZAZI/ MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi (Jina la mzazi/mlezi) ……………………………………………………………. Ambaye ni Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi) ……………………………………………………….. nimeyasoma na nimekubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ya Sekondari Julius Kambarage Nyerere ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

Aidha naahidi kuwa nitamlipia na kumpatia mwanangu huduma muhimu za shule kama vile; Michango ya shule, Sare za shule na michezo; Matibabu; Vifaa vya kujifunzia ikiwa ni pamoja na madaftari, kalamu, vitabu n.k

Jina la Mzazi/Mlezi …………………………….;.….. Namba ya simu …………………

Mtaa (Kitongoji) …………………………………………….. Kijiji …………………….

Anuani: S.L. P ………………………………………. Wilaya …………………………….

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………… Tarehe …………………………..